# Dawa ya Maambukizo Fiche ya TB Isoniazid (INH)

Utakunywa dawa yako mara moja kwa siku kwa miezi 9.

Utameza vidonge vyako vya kila siku pamoja kwa wakati mmoja.


Waambie madaktari wako wengine kwamba unatumia dawa ya maambukizo fiche ya TB.

| Dawa | Idadi ya vidonge kwa siku |
| --- | --- |
| Isoniazid | |

**Nitakunywa dawa yangu kila siku kwa miezi 9**

Public Health
Seattle & King County

TB FREE KING COUNTY



Una maambukizo fiche ya TB, aina ya maambukizo ya TB. Huna ugonjwa wa TB na huwezi kueneza TB kwa watu wengine. Dawa hii itasaidia kuzuia ugonjwa wa TB amilifu.



Piga simu muuguzi wako ikiwa una maswali au madhara:

______________

# ACHA

ACHA kutumia dawa zako mara moja na UPIGIE SIMU muuguzi wako wa TB ikiwa una matatizo yoyote kati ya yafuatayo:

- Hamu kidogo au hakuna hamu ya chakula
- Kuumwa kwa tumbo au mkakamao wa misuli ya tumbo
- Kichefuchefu ama kutapika
- Mkojo wa rangi ya kola au vinyesi vyepesi
- Ngozi au macho ya manjano
- Upele au kuwashwa
- Kuwashwa au kufa ganzi katika mikono au miguu yako

TB FREE KING COUNTY

## Vidokezo vya kutumia INH

- Weka king'ora ili kukukumbusha kunywa dawa yako
- Mwombe mtu wa familia au rafiki ili akukumbushe
- Ongea na daktari wako ikiwa unakuywa pombe, pombe inaweza kusababisha madhara
- Mwambie daktari wako kuhusu dawa nyingine ambazo unatumia
- Mwulize muuguzi wako ikiwa una maswali

Public Health
Seattle & King County